


**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 5, Issue 2, 2022**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EANSO
EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Wingilugha na Maendeleo Endelevu katika Kaunti Nchini Kenya: Hali Halisi katika Kaunti ya Machakos

*Peter Willington Kilonzo[1]* & Dkt. Nabeta Sangili, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Marafiki cha Kaimosi, S. L.P. 150 – 50309, Tiriki Kenya.
* Barua pepe ya mawasiliano: willingtonpeterk@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.991**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*04 Desemba 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*Wingilugha, Maendeleo Endelevu, Kaunti, Mtagusano.*

**IKISIRI**

Ulimwenguni kote, lugha imekuwa na bado inaendelea kuwa raslimali muhimu katika maendeleo ya sehemu yoyote ile. Kwa watu wengine, lugha ni mtaji katika shughuli zozote za kimaendeleo kwa sababu bila lugha inayoeleweka na washiriki husika hakuna maendeleo yanayoweza kupatikana na iwapo yatafanyika, kasi yake itakuwa ya chini sana. Katiba ya 2010 ilifanya mabadiliko mengi na mojawapo ni kukifanya Kiswahili kuwa lugha rasmi sawa na Kiingereza. Katiba hii pia ilitengeneza serikali 47 za magatuzi ambazo zina upekee wake wa utamaduni, lugha ikiwa sehemu muhimu ya utamaduni wa Kaunti hizi. Hivyo, angalau kila Kaunti ina lugha tatu zinazozungumzwa humo. Zaidi ya lugha husika tatu, shughuli tofauti zimechangia watu wa jamii mbalimbali kuhamia na kutagusana katika Kaunti tofauti na za kwao, jambo linalosababisha wingilugha dhahiri katika Kaunti zote nchini Kenya. Katika hali hii, swali kuu linakuwa ni: je, lugha ikiwa ni raslimali na mtaji muhimu katika maendeleo, wingilugha unaweza kutumika vipi katika muktadha wa Kaunti ili kuhakikisha maendeleo endelevu? Swali hili linakuwa msingi mkuu wa makala haya kuangazia jinsi wingilugha (Kiswahili, Kiingereza, Lugha asili, na lugha nyinginezo) unavyoweza kutumika katika muktadha wa Kaunti nchini Kenya ili kuhakikisha maendeleo endelevu katika kila Kaunti. Utafiti umejikita katika Kaunti ya Machakos.

**APA CITATION**

Kilonzo, P. W. & Sangili, N. (2022). Wingilugha na Maendeleo Endelevu katika Kaunti Nchini Kenya: Hali Halisi katika Kaunti ya Machakos. *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(2), 78-84. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.991.

**CHICAGO CITATION**

Kilonzo, Peter Willington and Nabeta Sangili. 2022. "Wingilugha na Maendeleo Endelevu katika Kaunti Nchini Kenya: Hali Halisi katika Kaunti ya Machakos". *East African Journal of Swahili Studies* 5 (2), 78-84. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.991.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.991

**HARVARD CITATION**

Kilonzo, P. W. & Sangili, N. (2022) "Wingilugha na Maendeleo Endelevu katika Kaunti Nchini Kenya: Hali Halisi katika Kaunti ya Machakos", *East African Journal of Swahili Studies*, 5(2), pp. 78-84. doi: 10.37284/jammk.5.2.991.

**IEEE CITATION**

P. W. Kilonzo & N. Sangili "Wingilugha na Maendeleo Endelevu katika Kaunti Nchini Kenya: Hali Halisi katika Kaunti ya Machakos", *EAJSS*, vol. 5, no. 2, pp. 78-84, Dec. 2022.

**MLA CITATION**

Kilonzo, Peter Willington & Nabeta Sangili. "Wingilugha na Maendeleo Endelevu katika Kaunti Nchini Kenya: Hali Halisi katika Kaunti ya Machakos". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 2, Dec. 2022, pp. 78-84, doi:10.37284/jammk.5.2.991.

## UTANGULIZI

Pengine istilahi ya *wingilugha* katika msimbo wa Kiswahili ni geni kwa watu wengi hata katika mataifa ya Afrika Mashariki ambako matumizi ya Kiswahili yamepanuka sana ikilinganishwa na maeneo mengine ulimwenguni. Hata hivyo, dhana yenyewe si geni katika ulimwengu wa sasa kutokana na mtagusano wa lugha takriban elfu tano zinazozungumzwa ulimwenguni kijamii au kitaifa kama anavyosema Crystal (2010). Lugha huwa ni nyenzo muhimu katika harakati za kuzalisha mali na uchumi wa eneo lolote ulimwenguni. Kulingana na Kawonga (2019), lugha ni mtaji kwa lengo la kupata faida katika harakati za kiuchumi. Kulingana na Pendakur na Pendakur (2015), lugha si lugha tu ya kuzungumza bali ni rasilimali muhimu katika maendeleo. Kwa kuzingatia maoni ya wataalamu hawa, lugha ni sawa na fedha, wafanyikazi, na hata teknolojia katika mchakato wa maendeleo. Kwa kuzingatia nafasi ya lugha kati ya raslimali hizi zote, utafiti huu unaiona lugha kama rasilimali kuu zaidi ya zote kwa sababu mawasiliano ni muhimu ili zote zitumike ipasavyo. Katika msingi huu, swali kuu linakuwa: je lugha zinapokuwa mbili au tatu au hata zaidi, yaani wingilugha, hali huwa vipi kimaendeleo? Matapo mawili yamejadili wazo hili la wingilugha na maendeleo. Tapo la kwanza linaona wingilugha kama shida na lingine linauona kama suluhisho la matatizo ya kimaendeleo. Nchini Kenya, Katiba ya 2010 ilirasimisha lugha ya Kiswahili kama ilivyo ya Kiingereza na kuunda serikali za Kaunti zenye upekee wa kiisimu. Mabadiliko haya mawili ya kikatiba yalipelekea uwepo wa wingilugha katika Kaunti zote arobaini na saba, hali ambayo inaendelezwa hata zaidi na shughuli mbalimbali za kimaendeleo kama vile ajira na biashara kwa kutaja tu chache. Makala haya yanadadisi pande hizi mbili za wingilugha na kuonyesha kwa kutoa mifano jinsi wingilugha unaweza kuchangia maendeleo endelevu katika muktadha wa Kaunti nchini Kenya.

## MAENDELEO ENDELEVU

Wakati jina *maendeleo* linapotajwa, wazo la kwanza kuingia akilini mwa wasikilizaji huwa ni ukuaji wa uchumi, ambalo ni wazo la ukweli. Lakini, swali kuu ni je, maendeleo yanahusisha ukuaji wa uchumi pekee? Saidi (2021) anafafanua maendeleo kuwa mchakato mseto wa kadri unaojumuisha upangaji upya wa mifumo yote ya kiuchumi na kijamii. Hivyo, maendeleo sio tu ya uchumi peke yake bali pia mawanda mengine ya kijamii. Akimnukuu Murdoch (1980), Saidi (2021) anasema kuwa maendeleo hayahusishi tu ukuaji wa uchumi, bali pia uboreshaji wa maisha ya umma, ujumuikaji katika uchumi ulio bora kimuundo na kiteknolojia, na ujenzi wa uchumi ambao una muundo wa kudhibiti ukuaji na kuzidi kuwa bora. Katika maelezo haya, dhana ya uendelevu ni kina katika maendeleo kwa sababu mojawapo ya vipengele hivi vinahusisha ukuzaji wa uchumi ambao muundo wake una uwezo wa kudhibiti ukuaji na ongezeko la ubora. Hivyo, maendeleo endelevu sio tu kukamilisha mradi mmoja kikamilifu kwa kiwango cha juu cha ubora bali kuhakikisha kuwa miradi ya baadaye inatimika kwa kiwango cha juu. Kipengele kingine ambacho kinajumuisha maendeleo kama inavyofafanua dhana hii ni kuwa maendeleo yanastahili kuhakikisha upungufu wa ukosefu wa usawa na kumaliza umaskini katika jamii.

Saidi (2021) anaendeleza maelezo ya dhana ya maendeleo kwa kumnukuu Rodney (1989) anayefafanua kuwa maendeleo katika kiwango cha mtu binafsi humaanisha kuwa na uwezo na stadi zaidi, ubunifu, uhuru zaidi, uwajibikaji, nidhamu, na uwezo na bidhaa tofauti. Akifafanua maoni haya ya mtaalamu huyu, Saidi anasema kuwa katika

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.991

maendeleo haya, mtu hutakikana kuwa na stadi zinazozaa uwezo wa kiuchumi, stadi ambazo hufunzwa katika lugha anayoielewa. Makala hii inakubaliana na wazo hili kabisa kuwa lugha inayoeleweka na walengwa wa maendeleo ni msingi wa kuhakikisha wana stadi zinazohitajika kuhakikisha maendeleo endelevu katika Kaunti zote nchini Kenya. Sehemu inayofuata inajadili lugha na maendeleo.

## Lugha na Maendeleo

Wataalamu tofautitofauti wameonyesha uhusiano mkubwa kati ya lugha na maendeleo. Jain (2011) anasema kuwa lugha ni sifa ya kijamii yenye umuhimu bia katika kuamua matokeo ya kiuchumi na kuwa wafanyikazi ambao wana uzoefu wa lugha kuu ya eneo maalumu hupokea mapato ya juu ikilinganishwa na wale ambao hawana. Kwa mujibu wa Chhaya (2017) akiwanukuu Halliday na Hymes, lugha katika maendeleo huzingatia kutatua matatizo yanayohusiana na lugha katika muktadha wa maendeleo ya watu binafsi au ya kijamii ambapo lugha hufafanuliwa kama umilisi wa kimawasiliano na maendeleo kama upunguzaji wa kuathirika kwa washiriki kutokana na vitu ambavyo hawawezi kuvidhibiti.

Mkwinda-Nyasulu (2013) anapojadili jukumu la lugha katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi anasema kuwa haiwezekani kusisitiza kupita kiasi jukumu la lugha katika maendeleo kwa sababu ukweli ni kuwa pale pasipo na lugha hakuna maendeleo. Hali hii inatokea kwa sababu kusudi la msingi la lugha ni mawasiliano ambayo ni kipengele muhimu cha kupata maendeleo pale ambapo inaonekana kama njia ya kufikia malengo yaliyowekwa bali si kama mwisho wa maendeleo.

Uhakiki wa fafanuzi hizi za uhusiano wa lugha na maendeleo zinaonyesha misingi mikuu ya kuelewa nafasi ya lugha katika maendeleo. Kwanza, lugha kama sifa ya kijamii yenye umuhimu bia katika kuamua matokeo ya kiuchumi ina maana kwamba lugha, iwe geni au asili, kongwe au changa, katika sehemu yoyote ya ulimwengu na jamii yoyote, iwe kati ya mataifa yaliyoendelea, yanayoendelea, na ambayo hayajaendelea ni msingi mkuu wa maendeleo. Pili, lugha ni nyenzo ya kutatua matatizo mengi yanayojitokeza katika mchakato wa maendeleo na tatu ni kuwa lugha ni msingi mkuu wa maendeleo kwa sababu bila lugha hakuna maendeleo. Pengine, katika msingi huu itakuwa kweli kusema kuwa lugha inaweza kupatikana na kuendelezwa bila maendeleo lakini maendeleo hayawezi kupatikana na kuendelezwa bila lugha. Hivi kwamba, katika mchakato wa maendeleo, maendeleo ni kigeu tegemezi na huku lugha ikiwa kama kigeu huru. Hata hivyo, ieleweke kwamba katika kujenga uhusiano huu, wataalamu hawa wote wanazungumzia lugha tu kwa ujumla na hivyo ni haki kuhitimisha kuwa kila lugha inayozungumzwa na watu wa eneo fulani ina nafasi maalumu katika maendeleo ya eneo hilo husika. Hata hivyo, hitimisho hili linazua swali la hali katika mazingira ya wingilugha. Hebu tuangaize uhusiano wa lugha na maendeleo katika mazingira haya ya wingilugha.

## Wingilugha na Maendeleo

Uhusiano kati ya wingilugha na maendeleo ni mmoja ambao katika ulimwengu wa uchumi umejadiliwa kutoka kwa mikabala miwili tofauti kabisa hasa barani Afrika: hasi na chanya. Kanana (2013) anasema kwamba Simpson anaeleza kwa usahihi matatizo ya lugha barani Afrika anaposema kuwa katika juhudi za kijumla za kujenga serikali mpya zilizo imara na zinazofungamana katika Afrika ya Sahara iliyo na wingilugha dhabiti na makabila mengi, lugha imethibitika kuwa nguvu muhimu. Anaendelea kusema kuwa lugha inaungana kwa karibu na ufikiaji wa elimu na wananchi, ajira, na ushiriki katika siasa na kwa ukuaji mpana wa hisia za pamoja za jamii ya kitaifa, jambo ambalo limepelekea kuzuka kwa hisia za wingilugha kama hali tata kwa maendeleo ya kitaifa badala ya rasilimali ya kutumiwa. Kauli hii ya Simpson ilimpelekea Kanana kuhitimisha kuwa wingilugha umeonekana kama shida badala ya raslimali ya kutumiwa kuendeleza umoja ndani ya uanuwai. Hivyo, wingilugha barani Afrika una uwezo wa kuleta maendeleo au kudidimiza maendeleo kutegemea jinsi ambavyo unatumika. Pale ambapo wingilugha unaonekana kama shida ambayo ilitokana na wakoloni, maendeleo yatazidi kuathirika vibaya. Lakini, pale ambapo wingilugha utaonekana kama rasilimali, kasi ya juu ya maendeleo itafikiwa. Ufumbuzi wa Walsh (2006) katika Kiunzi chake cha Kinadharia cha Lugha na Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi wa fomyula ya lugha tatu katika maeneo yenye wingilugha kama njia ya kuhakikisha maendeleo ya eneo husika-

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.991

yaani, lugha ya kimataifa, lingua franka ya kitaifa na lugha asili ni kina sana katika mjadala huu wa wingilugha na maendeleo. Pale ambapo lugha hizi tatu zinapojitwika majukumu maalumu katika jamii, maendeleo yanaweza kupatikana kwa kasi ya juu ikilinganishwa na kuishi katika dunia ya lawama kwa wakoloni na baadhi ya watu na ukengeushaji wa matumizi ya lugha za kikoloni kwa wengine.

Utwikaji wa majukumu kwa lugha tofauti katika mazingira ya wingilugha yameonekana kuzaa matunda ya kimaendeleo katika maeneo mbalimbali ulimwenguni na mfano mzuri ni nchini India.

Nchini India, iliyo na zaidi ya lugha mia moja na lugha rasmi ishirini na mbili, lugha hutwikwa majukumu mbalimbali. Hali ambayo Sridhar (1996) anasema imechangia maendeleo nchini humo. Kwa mfano, katika eneo dogo la Karnata, lugha tofauti zinatumika katika mawanda tofautitofauti ya kimaendeleo.

## WINGILUGHA NA MAENDELEO KATIKA KAUNTI, NCHINI KENYA: HALI YA MACHAKOS

Kama ilivyo nchini India, Kenya ina ‘mataifa’ madogo ambayo katika katiba ya 2010 yanatambulika kama Kaunti. Vilevile, Kaunti hizi zina upekee wa kiisimu kwa sababu Kaunti tofautitofauti zina lugha asilia tofautitofauti. Katiba hii pia ilirasimisha lugha ya Kiswahili kama kilivyo Kiingereza kando na kubaki kuwa lugha ya taifa. Mabadiliko haya ya kikatiba yalipelekea wingilugha rasmi katika kila mojawapo ya Kaunti arubaini na saba za taifa la Kenya. Makala haya yaakisi kuwa kama ilivyo nchini India, wingilugha unaweza kuleta maendeleo katika Kaunti hizi hata zikiwa na tofauti za kiisimu. Hebu tuangazie hali katika Kaunti ya Machakos kama mfano ambako utafiti halisi ulifanywa kuchunguza wingilugha na athari zake kwa utekelezaji wa maendeleo.

Katika utafiti huu, maeneo lengwa yalihusisha vijiji sita ambavyo vina wingilugha dhahiri kutokana na uzingasifa. Maeneo vizingasifa, yalihusisha mazingira mawili; ya mijini na mashambani. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kuwa watu wanaoishi katika maeneo haya ni wa viwango tofauti vya umri na elimu. Vilevile, watu wa maeneo haya hushiriki katika shughuli tofautitofauti za kimaendeleo. Kitakwimu, vijana (miaka 18-35) walihusisha asilimia 32.2, umri wa makamo (36-45) asilimia 34.8, na wazee (zaidi ya miaka 46) walikuwa asilimia 33.0. Vilevile, kwa kuzingatia kiwango cha elimu, asilimia zifuatazo za watu wako katika viwango hivi:

**Jedwali 1: Viwango vya elimu ya watafitiwa**

| | Mdafao | Asilimia |
|---|---|---|
| Sijawahi Kusoma | 5 | 4.3 |
| Darasa la 8 | 32 | 27.8 |
| Kidato cha nne | 45 | 39.1 |
| Chuo cha Kati/Kikuu | 33 | 28.7 |
| Jumla | 115 | 100.0 |

Wale ambao hawajawahi kusoma walikuwa 4.3% na ndio waliorekodi asilimia ya chini kabisa. Hata hivyo, asilimia hii ilitambua uwepo wa watu wa aina hii katika Kaunti sio tu ya Machakos lakini pia Kaunti nyingine, jambo ambalo ni kina kulitambua ili kutumia lugha kwa namna inayowahusisha ili kuhakikisha maendeleo endelevu. Walifuatiwa na waliosoma hadi darasa la nane kwa asilimia 27.8 ambao nao walifuatiwa kwa karibu na waliosoma hadi vyuo vya kati na vikuu kwa asilimia 28.7. Waliosoma hadi kidato cha nne ndio walikuwa wengi zaidi kwa asilimia 39.1. Takwimu hizi ni muhimu kwa sababu zinatambua uwepo wa viwango vyote vinne vya elimu katika muktadha wa Kaunti ambao ni muhimu katika kuhakikisha lugha inatumiwa kwa namna itakayohakikisha kuwa washiriki wa viwango hivi vyote wanapata maendeleo, jambo lililo muhimu kuhakikisha maendeleo endelevu.

Matokeo yalionyesha kuwa wananchi walifanya kazi mbalimbali katika Kaunti ya Machakos kama ifuatavyo:

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.991

**Jedwali 2: Kazi za watafitiwa**

| | Mdafao | Asilimia |
|---|---|---|
| Ofisini | 12 | 10.4 |
| Nyumbani | 14 | 12.2 |
| Shambani | 21 | 18.3 |
| Hospitalini | 6 | 5.2 |
| Biashara | 38 | 33.0 |
| Sehemu Nyingine | 24 | 20.9 |
| Jumla | 115 | 100.0 |

Kwa mujibu wa takwimu hizi, 10.4% ya watafitiwa walifanya kazi ofisini, 12.2% nyumbani, 18.3% shambani, 5.2% hospitalini, 33.0%, ambayo ndiyo asilimia kubwa zaidi, walikuwa wanabiashara na 20.9% katika sehemu nyingine.

Vilevile, matokeo yalionyesha kuwa zaidi ya lugha kumi zinazungumzwa katika Kaunti hii, hali ambayo imeletwa na urasmishwaji wa Kiswahili na Kiingereza, elimu, ndoa, kazi, biashara, ujirani na Kaunti zenye wakaazi wasio Wakamba, miongoni mwa sababu nyingine. Sababu hizi za wingilugha zinaonyesha hali katika Kaunti zote nchini Kenya na kuthibitisha kuwa kila Kaunti ina wingilugha ulio dhahiri kabisa.

Ukweli wa pendekezo la Walsh (2006) la matumizi ya fomyula tatu ya lugha katika mazingira ya wingilugha ulithibitika katika Kaunti ya Machakos kwa sababu lugha tatu zinatumika sana katika mchakato wa utekelezaji maendeleo. Lugha ya Kikamba ilichukua nafasi ya lugha asili, Kiswahili nafasi ya lingua franka ya kitaifa na Kiingereza kuchukua nafasi ya lugha ya kimataifa. Kikamba (lugha asili), kilitumika katika kuendeleza shughuli za utekelezaji maendeleo miongoni mwa wananchi wenyewe hasa wale wanaoishi katika maeneo ya mashambani. Hata pale washikadau wa maendeleo wanapowasilisha sera za maendeleo kwa wananchi wa maeneo haya, lugha ya Kikamba ilitumika zaidi ikilinganisha na lugha nyinginezo. Hali hii inaonyesha nafasi ya lugha asili katika maendeleo ya maeneo ya mashambani. Katika mahojiano na maafisa wakuu wa idara za Kilimo, Utamaduni, Nyumba na Ukuaji wa Miji, na Biashara, maafisa hawa katika vipindi tofauti vya mahojiano walikubaliana kuwa lugha ya kwanza ndiyo iliyo bora kabisa kuhakikisha wananchi wa mashambani wanaelewa michakato ya maendeleo.

Vilevile, lugha hii ya Kikamba inapendelewa zaidi na wazee na wale walio na kiwango cha chini cha elimu. Kaunti hii ya Machakos ni kielelezo kizuri cha nafasi ya lugha asili katika utekelezaji wa maendeleo katika maeneo ya mashambani. Zaidi, inathibitisha ukweli wa mhimili wa Kiunzi cha Kinadharia cha Lugha na Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi cha John Walsh kuwa mafunzo kwa lugha ya kwanza huchangia katika maendelezo ya vigezo vya kijamii, kitamaduni na kimaendeleo katika jamii. Kila Kaunti nchini Kenya, isipokuwa Kaunti ya Nairobi ina wananchi wanaoishi katika maeneo ya mashambani. Hivyo, lugha asili zina nafasi ya kuhakikisha kwamba stadi mbalimbali za maendeleo zinaeleweka kwa usahihi zaidi. Hali itayohakikisha upitishaji wa stadi hizi kutoka kizazi kimoja hadi kingine na hivyo kuhakikisha maendeleo endelevu katika kila Kaunti.

Lugha ya Kiswahili, ambayo ni lingua franka ya kitaifa nayo iliibuka kuwa na nafasi kubwa sana katika maendeleo katika kiwango cha Kaunti. Katika Kaunti ya Machakos, lugha hii inatumika zaidi katika maeneo ya mijini ambako kuna watu kutoka jamii mbalimbali na vijiji ambako kuna watu wasioelewa lugha ya Kikamba na Kiingereza. Lugha ya Kiswahili ndiyo lugha inayounganisha jamii zote zinazoishi katika Kaunti ya Machakos, hali inayoendana na matokeo ya ufafanuzi wa Kanana (2013) kuwa ni lugha inayowaleta wananchi pamoja, hali inayopanua nafasi yao ya kushiriki katika maendeleo. Pendakur na Pendakur (2015) walionya kuwa wingilugha huwa na athari hasi pale ambapo lugha inatumika kuwabagua watu wa jamii moja katika shughuli za ajira, pengo ambalo lugha ya Kiswahili imeziba katika Kaunti hii, na ambayo inaziba katika Kaunti nyingine 46.

Kiswahili pia kina nafasi maalumu katika mawanda ya biashara kwa sababu wafanyibiashara wote

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.991

waliohusishwa katika utafiti huu walikiri kutumia Kiswahili katika maingiliano yao na wateja hasa katika maeneo ya mijini. Katika maeneo ya mashambani, Kiswahili ndiyo lugha wanayotumia wafanyibiashara wanapohudumia watu walio wageni. Matumizi ya Kiswahili, kwa mujibu wa wanabiashara hawa, huongeza idadi ya wateja kwa sababu inasaidia kuhudumia wateja wote sawa na kutengeneza uhusiano mwema na wale wa jamii nyingine. Matokeo ya matumizi ya Kiswahili katika biashara yalitokea kuwa ya juu zaidi, hali inayoongeza matokeo yao ya kiuchumi. Katika kilimo, lugha ya Kiswahili ilitumika sana katika mafunzo katika mazingira yaliyo na wakulima wa jamii tofautitofauti wasioelewa Kikamba. Ni lugha ambayo matumizi yake katika nyaraka za kilimo yanaendelea kupanuka kwa sababu uhakiki wa nyaraka 23 zenye maagizo ya kilimo ulionyesha kuwa asilimia 21.7 yazo zilikuwa kwa Kiswahili. Asilimia 60 ya hizi zilikuwa za Kiswahili peke yake na asilimia 40 zilikuwa za Kiingereza na tafsiri yake katika Kiswahili. Hali hii ni tofauti na awali ambapo lugha ya Kiingereza pekee imekuwa ikitumiwa katika nyaraka huku Kiswahili kikitumika katika mazungumzo yasiyo rasmi. Hali hii katika Kaunti ya Machakos inaonyesha nafasi ya lugha ya Kiswahili katika Kaunti zote nchini Kenya. Wingilugha katika Kaunti hizi ni jambo ambalo haliwezi kuepukika kwa sababu unasababishwa na mambo yaliyo juu ya mamlaka ya Kaunti zenyewe na hata serikali kuu. Hivyo, lugha ya Kiswahili inaimarisha usawa katika mchakato wa maendeleo, jambo analosisitiza Mudroch ndani ya Saidi (2021) kuwa sehemu ya kina katika maendeleo. Lugha ya Kiswahili ni kina cha kuhakikisha maendeleo endelevu katika muktadha wa Kaunti kwa sababu inawaunganisha wananchi wa viwango mbalimbali vya elimu, umri, jinsia, na hata kazi mbalimbali.

Kwa upande wa lugha ya Kiingereza, matumizi yake ni mapana sana miongoni mwa umri wa vijana, waliosoma hadi kiwango cha juu cha elimu, wanaofanya kazi katika mawanda rasmi kama vile hospitalini, na maeneo ya mijini. Hata hivyo, lugha ya Kiingereza bado ina nafasi katika maendeleo ya mashambani. Lugha hii hutumika zaidi mashambani katika mafunzo ya kilimo na mengine pale ambapo istilahi maalumu zinaeleweka kwa urahisi kutumia Kiingereza. Kwa mfano, katika mahojiano na Afisa Mkuu katika Idara ya Kilimo katika Kaunti ya Machakos, alisema kuwa lugha ya Kiingereza hutumika katika mafunzo ya kilimo katika baadhi ya maneno kama vile mbolea za DAP na CAN ambazo istilahi zake kwa Kiswahili hazipo au hazijulikani. Utafiti huu uligundua kuwa lugha ya Kiingereza ni maarufu sana katika mazingira rasmi ambayo ndiyo mazingira ambamo sera za maendeleo huundiwa. Zaidi ni lugha rasmi na wananchi kwa mujibu wa katiba wana uhuru na haki ya kuitumia mahali popote wakati wowote kadri ya uwezo wao. Isitoshe, Kaunti ya Machakos ina wafanyibiashara wa kigeni kama vile Waarabu, Wahindi na Wazungu ambao hawaelewi lugha ya Kiswahili. Wengine huja kwa shughuli za muda mfupi kama vile mafunzo ya kilimo na afya ambayo ni muhimu katika kuhakikisha maendeleo endelevu. Katika maingiliano na wageni hawa, lugha ya Kiingereza hutumika zaidi. Hata hivyo, ili kuhakikisha mawasiliano sahihi na wananchi, huduma za ukalimani hutumika ili kuziba pengo hili la kimawasiliano. Matokeo haya ya matumizi ya Kiingereza katika Kaunti ya Machakos yanaonyesha nafasi ya matumizi ya lugha ya Kiingereza katika muktadha wa Kaunti nchini Kenya katika kuhakikisha maendeleo endelevu. Lugha nyingine asili hutumika katika mazungumzo miongoni mwa watu wa jamii mbalimbali.

## HITIMISHO

Makala haya yanaonyesha kwa kina zaidi kuwa wingilugha ni raslimali kubwa katika mchakato wa maendeleo katika Kaunti za Kenya kwa wakati wa leo. Japokuwa kuna wasomi ambao wamependekeza matumizi ya lugha asilia kama njia ya kuhakikisha maendeleo ya maeneo mbalimbali kama vile Kanana (2013), Saidi (2021), Chhanya (2017), makala haya yanaonyesha kuwa wingilugha bado una nafasi kubwa katika mchakato wa kuhakikisha maendeleo endelevu. Baadhi yao hawakubaliani na lawama kuwa lugha asilia kama vile Kiswahili hazina msamiati wa kutosha kwa sababu istilahi za baadhi ya vitu hazipo na kupendekeza lugha hizi kuanza kutumika jinsi zilivyo, wazo ambalo kwao litasaidia kuunda istilahi husika. Makala hii inakubaliana na maoni yao kwa asilimia mia moja. Hata hivyo, maendeleo yataathirika kwa namna hasi iwapo yatakwepa matumizi ya lugha ya Kiingereza wakati tunapokuza matumizi ya lugha hizi asilia. Hivyo, ili kuhakikisha maendeleo endelevu katika muktadha wa Kaunti nchini Kenya, wingilugha una nafasi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.991

kubwa katika kuhakikisha mawasiliano na mafunzo ya stadi maalum zinazohitajika kuhakikisha maendeleo yanafanyika kwa lugha inayoeleweka kabisa na wananchi wenye sifa maalumu kwa wakati wowote ule.

## MAREJELEO


Chhaya, K. S. (2017). 'Economic development and language: A journey through India'. *SSRN Electronic Journal*. https://doi.org/10.2139/ssrn.3053765

Crystal, D. (2010) *The Cambridge Encyclopedia of Language*. Cambridge: Cambridge University Press.

Jain, T. (2011). Common tongue: The impact of language on economic performance. *SSRN Electronic Journal*. https://doi.org/10.2139/ssrn.1947148

Kanana, F. E. (2013). Examining African Languages as Tools for National Development: The Case of Kiswahili. *The Journal of Pan African Studies*, *6*(6), 41-68.

Kawonga, G. A. (2019). *Nafasi ya Kiswahili katika mandhari-lugha: Uchambuzi kifani wa mabango ya matangazo ya makampuni ya mawasiliano ya simu*. Apache Tomcat/8.5.60. https://ir.mu.ac.ke:8080/xmlui/handle/123456789/3779

Mkwinda-Nyasulu, B. (2013). Role of language in socio–economic development: the semiotics are right. *Journal of Humanities*, *23*, 213-230. https://www.ajol.info/index.php/jh/article/view/151922/141518

Pendakur, K., & Pendakur, R. (2015). Speak and Ye Shall Receive: Language Knowledge as Human Capital. In *Economic Approaches to Language and Bilingualism. New Canadian Perspectives* (1st ed., pp. 89-120). EDRS.

Saidi, M. V. (2021). Kiswahili na Maendeleo Mashambani nchini Kenya. *Jarida la CHAKITA*, *1*(1), 19-26.

Sridhar, K. K. (2006). Societal Multilingualism. In *Sociolinguistics and Language Teaching* (11th ed., pp. 47-70). Cambridge University Press.

Walsh, J. (2006). *Language and socio-economic development. Towards a Theoretical Framework*, *30*(2), 127-148. https://doi.org/10.1075/lplp.30.2.03wal


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.